# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA NANE

## KIKAO CHA KUMI

**10 FEBRUARI, 2025**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA NANE

## KIKAO CHA KUMI – TAREHE 10 FEBRUARI, 2025

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA (PIC):**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2024.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2024.

## III. MASWALI:

## OFISI YA WAZIRI MKUU:

**158. MHESHIMIWA NICODEMAS HENRY MAGANGA (MBOGWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, lini Serikali itafanya mabadiliko kwenye Kikokotoo cha Watumishi nchini kwa kuwa kumekuwa na malalamiko mengi.

**159. MHESHIMIWA TOUFIQ SALIM TURKY (MPENDAE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, kuna mpango gani wa kuwaandaa Vijana kushindana katika soko la ajira ndani na nje ya Tanzania ili kukabiliana na upungufu wa ajira nchini.

## OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**160. MHESHIMIWA MARY FRANCIS MASANJA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali haioni haja ya kuanzisha Halmashauri katika Jiji la Mwanza kwa kuwa linazidi kupanuka.

**161. MHESHIMIWA DKT. CHRISTINE GABRIEL ISHENGOMA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Kituo cha Afya Magubike – Kilosa.

**162. MHESHIMIWA DKT. RITTA ENESPHER KABATI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Makaravati na Madaraja madogo yatajengwa katika Barabara ya Itimbo Kitelewasi.

**163. MHESHIMIWA BONIPHACE NYANGINDU BUTONDO (KISHAPU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itapeleka fedha za dharura Wilayani Kishapu ili kufanya matengenezo ya Barabara zilizoharibiwa na Mvua za Elninyo Mwaka 2023/24.

**164. MHESHIMIWA ABDALLAH JAFARI CHAUREMBO (MBAGALA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Barabara za Chasimba, Cheketu, Kisiwani, Alfurkan, Kwa Kisauti, Maduka Manane, Kwa Mnyani, Fella Zahanati na Ofisi ya Mtaa zitajengwa.

## OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UWEKEZAJI):

**165. MHESHIMIWA ORAN MANASE NJEZA (MBEYA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mipango na Uwekezaji):-

Je, kuna mkatati gani wa matumizi endelevu ya Kiwanda na Mashamba ya iliyokuwa Tanganyika *Packers Ltd* katika Mji wa Mbalizi.

## WIZARA YA NISHATI:

**166. MHESHIMIWA NEEMA KICHIKI LUGANGIRA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, Serikali haioni haja kupitia upya Mkataba wa REA kuhakikisha umeme unafikishwa mashuleni ili shule ziunganishwe na huduma za TEHAMA.

**167. MHESHIMIWA KABULA ENOCK SHITOBELA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini Serikali itatoa ruzuku ya Nishati Safi ya kupikia ili kuwasaidia Akina Mama wasifanyiwe ukatili na kuuawa kutokana na imani potofu.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**168. MHESHIMIWA ATUPELE FREDY MWAKIBETE (BUSOKELO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Serikali itatoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Polisi Kandete - Busokelo.

**169. MHESHIMIWA SUMA IKENDA FYANDOMO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Vituo vya Polisi vilivyojengwa kwa nguvu za Wananchi - Mbeya.

**170. MHESHIMIWA DOROTHY GEORGE KILAVE (TEMEKE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Serikali itaendelea kujenga nyumba za Askari Polisi eneo la Kilwa Road Jimbo la Temeke.

**WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:**

**171. MHESHIMIWA MARIAM MADALU NYOKA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza Bajeti ya Mikopo ya Makundi Maalum kwa kuwa uhitaji ni mkubwa.

**WIZARA YA MAJI:**

**172. MHESHIMIWA JOSEPHINE JOHNSON GENZABUKE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itamaliza tatizo la upungufu wa maji katika Kijiji cha Kabulanzwili - Kigoma.

**WIZARA YA KILIMO:**

**173. MHESHIMIWA DKT. JOHN DANIELSON PALLANGYO (ARUMERU MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kufufua Kilimo cha Pareto Kisimiri Juu ili Wananchi wa eneo hilo wanufaike kama ilivyokuwa miaka ya nyuma.

**WIZARA YA FEDHA:**

**174. MHESHIMIWA HASSAN SELEMAN MTENGA (MTWARA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, Iini Serikali itarejesha makusanyo ya Kodi ya Ardhi ya asilimia 20 kwa Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara Mikindani.

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

**175. MHESHIMIWA MAIMUNA AHMAD PATHAN (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

Je, lini Serikali itamaliza migogoro ya ardhi kati ya Wakulima na Wafugaji maeneo ya Liwale, Kilwa, Nachingwea na Lindi Vijijini.

**WIZARA YA MADINI:**

**176. MHESHIMIWA MRISHO MASHAKA GAMBO (ARUSHA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:-

Je, lini Serikali itaruhusu kuuzwa Tanzanite kwenye Masoko ya Madini ya ndani ya Arusha, Mwanza, Mbeya, Dar es Salaam na Zanzibar.

**177. MHESHIMIWA ALLY MOHAMED KASSINGE (KILWA KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:-

Je, Serikali imefikia hatua gani katika mchakato wa ujenzi wa Kiwanda cha Chumvi eneo la Nangurukuru – Kilwa.

## IV. HOJA ZA KAMATI:

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA (PIC):**

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2024.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:**

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2024.

| | |
|---|---|
| **DODOMA** | **BARAKA I. LEONARD** |
| **10 FEBRUARI, 2025** | **KATIBU WA BUNGE** |